**MULIKA Na. 40(1) 2021 (108-125)**

# Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili

*Aginiwe Nelson Sanga*[1]

Chuo Kikuu cha Dodoma

## Ikisiri

Kuibuka kwa mijadala kuhusu ujumi wa Kiafrika katika nyuga mbalimbali ukiwamo uga wa fasihi, kumechangiwa na mahusiano ya kihistoria ya Waafrika na watu wa mataifa mengine, hususani watu kutoka jamii za Kimagharibi. Kwa karne nyingi Waafrika wameonekana ni jamii ya watu duni, washenzi, washirikina na kwamba Afrika hakuna chochote chenye maana wala chenye kuvutia (Neugebauer, 1991). Mitazamo ya namna hiyo katika kutathmini ulimwengu wa Kiafrika haijaishia kwa wageni tu, bali hata baadhi ya Waafrika walioathiriwa na elimu ya Kimagharibi huuzungumzia utamaduni wa Kiafrika na fasihi yake kwa namna hiyohiyo. Hili linadhihirika bayana pale tunapoona fasihi simulizi ya Kiafrika ikiwamo fasihi simulizi ya Kiswahili inapigwa kumbo na Waafrika wenyewe katika maeneo mbalimbali muhimu ya kijamii (Sanga, 2018). Makala haya yamechambua hadithi fupi simulizi kama sehemu ya fasihi simulizi ya Kiswahili ili kuonesha thamani za ujumi wa Kiafrika kwa ustawi wa jamii za Kiafrika. Utafiti uliozalisha makala haya ulikuwa wa kimaktaba na uwandani. Aidha, data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uchanganuzi matini na mahojiano. Utafiti ulitumia mkabala wa kitaamuli katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Aidha, data hizo pia zilichanganuliwa kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Ujumi Mweusi.

## 1.0 Utangulizi

Kukithiri kwa maingiliano ya wanajamii na tamaduni za jamii mbalimbali duniani kulikowezeshwa na utandawazi, kumedumaza na kukengeusha fasihi simulizi asilia za mataifa mbalimbali, hususani yale yanayoendelea. Bello (2010) anaeleza kuwa kwa kiasi kikubwa utamaduni wa jamii za sasa katika Afrika umesheheni Umarekani, na Afrika yenye utajiri mkubwa wa utamaduni inaonekana kutoambulia kitu. Hii ni kwa sababu utamaduni wake, ikiwamo fasihi simulizi

[1] **Baruapepe:** vogosivopala@gmail.com

inaonekana ni ya watu dhalili inapolinganishwa na utamaduni wa mataifa yenye nguvu. Makala haya yanakusudia kujadili thamani ya ujumi wa Kiafrika kama inavyojitokeza katika hadithi fupi simulizi za Kiswahili kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Ujumi Mweusi. Hata hivyo, kabla ya kuendelea na vipengele vinavyofuata litakuwa jambo jema ikiwa tutaanza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana za msingi kama zilivyotumika katika makala haya.

Hadithi fupi ni utanzu unaohusisha hadithi fupi simulizi (masimulizi ya kimapokeo ambayo huhifadhiwa kichwani na kutolewa kwa mdomo ambayo kwa nyakati za sasa huwasilishwa katika maandishi na katika njia nyingine za kisasa), na pia utanzu wa hadithi fupi andishi. Hivyo, utanzu wa hadithi fupi ni utungo wa kinathari unaosimulia kisa au tukio kwa kujigeza katika ufundi wa kutumia lugha kwa ubanifu. Ubanifu huo hudhihirika katika wahusika, mandhari, wakati na visa vinavyosimuliwa. Usimulizi katika utanzu huu hauna utondoti wa kimaelezi kama wa riwaya; kinachotawala katika hadithi fupi ni mada kuu inayosimuliwa. Hadithi fupi andishi ni hadithi za kubuniwa ambazo siyo za kimapokeo zinazowasilishwa na kuhifadhiwa katika maandishi. Kwa mujibu wa Samwel (2012), hadithi fupi andishi za sasa zimekiuka sifa za hadithi fupi zinazobainishwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili kama vile kuwa na wahusika wengi, msuko wa visa changamani, urefu na mandhari inayoelezwa kikamilifu. Makala haya yamejikita katika uchambuzi wa hadithi fupi simulizi. Hadithi fupi simulizi ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi ya jamii ya Waswahili. Mulokozi (1996) ameainisha tanzu sita za fasihi simulizi ambazo ni semi, masimulizi, mazungumzo, ushairi simulizi, maigizo na ngomezi. Hadithi fupi simulizi zipo katika utanzu wa masimulizi ambao unajumuisha aina mbalimbali za hadithi fupi simulizi, aina za hadithi zilizojadiliwa katika makala haya ni: ngano, hekaya, hurafa, visakale na mbazi.

Ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo huwatumia wahusika wa aina mbalimbali kama vile wanyama, mimea, wadudu, au watu kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo kuhusu maisha. Kuna mitazamo tofauti ya wataalamu kuhusu aina hii ya hadithi: wapo wanaoona kuwa ngano ni kisawe cha hadithi fupi simulizi (za kimapokeo) (Senkoro, 2011; Wamitila, 2004) na wengine wanaona ngano ni aina mojawapo ya hadithi fupi simulizi (Madumulla, 2009; Mulokozi, 1996). Makala haya yamechambua ngano kama aina mojawapo ya hadithi fupi simulizi. Mbazi ni hadithi isiyokuwa ndefu inayotolewa katika maongezi ili kutoa mafunzo yenye uadilifu. Mbazi hujitokeza sana katika *Biblia* ambapo Bwana Yesu alitoa mafunzo kupitia mafumbo ya kisimulizi. Hekaya husimulia juu ya wahusika wajanja ambao aghalabu huwahadaa wahusika wengine na kunufaika. Baadhi yao hudanganyika na wahusika wajanja kuwapiku. Wahusika hao huweza kuwa ni wanyama, watu au mchanganyiko. Aghalabu hadithi hizi hujaa vichekesho na baadhi yake husimuliwa matukio halisi. Visakale ni masimulizi ya mapokeo juu ya wahenga au mashujaa wa kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia. Kwa mfano, hadithi ya *Lwanda Magere* wa kabila la Waluo, Kenya. Hurafa ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika wanyama kuelezea au kuonya kuhusu maisha.

Dhana ya ujumi katika makala haya inatazamwa kama tawi la falsafa linalojishughulisha na uzuri, ubaya, ladha, uchanya, uhasi, ubora na udhalili. Pia, inatazamwa kama taaluma inayohusu elimu ya sheria na kanuni za sanaa. Hivyo, ujumi ni uzuri, ubaya, ladha, uchanya, uhasi, ubora na udhalili wa kazi ya fasihi. Ujumi unajumuisha sheria na kanuni zinazopaswa kufuatwa ili kuunda kazi ya fasihi inayotazamwa kuwa "bora" katika jamii inayohusika.

Tunapozungumzia juu ya ujumi wa Kiafrika, ijapokuwa jamii za Waafrika zinatofautiana katika masuala kadhaa ya kiutamaduni, kihistoria, kiutawala, kiteknolojia na kimaeneo, yapo mambo ya jumla na ya kimtambuko yanayowatambulisha Waafrika wote likiwamo suala la uhakiki wa ujumi. Hakuna jamii duniani ambayo haina namna ya kuhakiki ujumi katika mazingira na katika utamaduni wake. Yakiwekwa kando masuala ya sanaa, Waafrika walitambua, walithamanisha na kuhakiki uzuri, ubaya, ubora na udhalili wa watu, mazingira, hali ya hewa, zana na vitu wanavyovitengeneza, matumizi ya lugha, mahusiano na miungu yao katika ulimwengu wao wanamoishi unaoonekana na usioonekana.

Kutokana na ufafanuzi huo wa ujumi katika makala haya, dhana ya ujumi wa Kiafrika inajumuisha mtazamo na tajiriba katika kuhakiki, kutambua, kutathmini uzuri au ubaya, ubora au udhalili, uhasi na uchanya wa kazi za sanaa za Waafrika kulingana na hali halisi ya ulimwengu wa Waafrika. Kwa Waafrika, sanaa haipo kwa kukidhi malengo yake yenyewe tu, bali hata hali halisi zilizopo katika mazingira yao na miktadha mbalimbali ya kijamii. Ujumi katika sanaa za Waafrika ni dhana inayotumika kuonesha sifa na vipengele muhimu vya idili za jamii vilivyosanifiwa katika maumbo mbalimbali ya sanaa. Vipengele hivyo ni pamoja na usawiri wa watu na maisha yao katika sanaa, usanifu wa maumbo yenyewe, ushababi na dhima za sanaa kwa jamii. Ujumi wa Kiafrika huhusisha pia vipengele vya kimaadili katika uhakiki wa uzuri, na lugha inayotumika katika kuthamanisha vitu na haitofautishi uzuri na wema. Uzuri au ubaya wa kazi za sanaa hutathminiwa pia kwa kuhusisha kipengele cha uwezo wa sanaa katika kuburudisha, na uwezo wa kufunza maadili kwa wanajamii. Masuala ya maadili na dini aghalabu huwa ndio maudhui ya msingi yanayobebwa na kazi za sanaa. Kazi za sanaa za Waafrika, kwa sehemu kubwa, zilionekana zikitumiwa katika miviga, sherehe, jandoni, makaburini na katika nyumba za watu kwa lengo la kukidhi haja za kiimani na kimaadili.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti uliozaa makala haya umeongozwa na Nadharia ya Ujumi Mweusi ambayo chimbuko lake ni katika vuguvugu la Unegritudi ambao ni vuguvugu la mabadiliko ya kiutamaduni lililotokea miaka ya 1930 huko Paris, Ufaransa. Unegritudi ulichochea hisia za watu weusi kutoka Afrika na nje ya Afrika kuthamini rangi na utamaduni wao (Berrian na Long, 1967). Uliwaamsha watu weusi katika kuhoji uhalali wa watu wa mataifa ya Magharibi kutawala nchi zao, kupinga ubaguzi wa rangi na kuuchambua utumwa na athari walizozipata (Sanga, 2012). Ndipo mwandishi na mhakiki Mganda, Zirimu (1973) akaibuka na Nadharia ya Ujumi Mweusi, akieleza kuwa ujumi ni vigezo vya kuuainisha

urembo wa sanaa na vigezo hivyo hutokana na hali halisi iliyopo katika jamii husika. Kila jamii ina ujumi wake. Jamii za kijamaa zina ujumi wa kijamaa, vivyo hivyo na jamii za kitabaka zina ujumi wenye tabia zinazothaminiwa na tabaka tawala. Zirimu anaona kuwa wahakiki wanaotumia mbinu za kigeni kuhakiki fasihi ya Kiafrika, siyo wahakiki halisi, ni waigaji. Uhakiki wenye kufaa ni ule unaoibuka katika jamii inayochambuliwa (Wafula na Njogu, 2007). Misingi ya nadharia hii imejikita katika mitazamo miwili ifuatayo: mosi, kwa kuwa ujumi ni taaluma inayohusika na sheria pamoja na kanuni za sanaa, kanuni hizo huundwa ndani ya jamii yenye kuumba kazi hizo. Pili, ingefaa watu wenye ufahamu na tajiriba ya kutosha kuhusu Afrika na Waafrika pamoja na utamaduni wao ndio wahusike kwa sehemu kubwa katika kutoa maamuzi ya kiujumi kuhusu uzuri au ubaya wa kazi za fasihi za Kiafrika.

## 3.0 Mbinu Zilizotumika Kukusanya Data

Utafiti uliozaa makala haya ulikuwa ni wa kitaamuli ambapo mwegamo wake ni wa kiufafanuzi kwa kuwa masuala ya tajiriba, mahusiano, mila na desturi, mitazamo na misukumo ya watu ndiyo yaliyochunguzwa na kufafanuliwa (Kothari, 2009). Pia, mbinu na njia zilizotumiwa katika kukusanyia data ni nusu funge na maswali ya utafiti hayakuwa kwa lengo la kupima idadi bali hali, tabia, mitazamo na tajiriba za jamii ya watoataarifa. Mbinu ya mahojiano na mbinu ya uchanganuzi matini ndizo zilitumika katika ukusanyaji wa data. Mbinu ya mahojiano imetumika katika kukusanya data za uwandani kwa wazee waliohojiwa katika vijiji vilivyopo wilayani Makete. Utafiti ulikusanya hadithi fupi simulizi tatu zilizochambuliwa katika makala haya kutokana na masimulizi ya watoataarifa wazee ambazo ni *Hadithi ya Kuchonga Meno*, *Ng'ombe na Ndama Wake* na *Lwembe*. Utafiti pia ulipata taarifa mbalimbali zinazohusiana na uamilifu wa hadithi fupi simulizi kiujumi katika jamii yao. Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumika katika uchambuzi wa hadithi simulizi za kimapokeo za maktabani zilizoandikwa katika vitabu (*Mzee Kobe na Sungura*, *Fisi na Rafiki Zake)* pamoja na hadithi tatu zilizosimuliwa na wazee uwandani, zilizotajwa hapo juu. Mwongozo wa uchanganuzi matini uliongoza katika uchambuzi wa kina uliofanyika kutoka matini moja hadi nyingine za hadithi fupi simulizi zilizokusanywa. Mwongozo wa uchanganuzi ulihusisha kategoria ya ujumi ya uzuri pamoja na mpinzani wake uwi ambapo vipengele vya ujumi wa Kiafrika vya umoja, ushababi, utu, ukizinda, makusudio, utii na adabu na imani za dini vilibainishwa kwa kila hadithi. Makala yamezichambua hadithi kwa kuzingatia maudhui yanayoendana na vipengele vya ujumi vilivyowekwa.

## 4.0 Vipengele vya Ujumi wa Kiafrika

Ujumi wa Kiafrika umefumbatwa na vipengele kadhaa ambavyo ni muhimu kuvifahamu, kwa kuwa ndivyo vinatambulisha na kuathiri utamaduni na maisha ya Waafrika kwa sehemu kubwa. Vipengele hivyo vya kiujumi huambatana na umbo la ndani la kazi ya fasihi. Vipengele vilivyojadiliwa katika makala haya ni kuishi kwa ushirika, utu, utii na adabu, makusudio, ushababi, ukizinda, na imani za dini. Mosi, kuishi kwa ushirika. Huu ni mfumo wa maisha ya ushirika kwa jamii za Waafrika unaojipambanua kupitia namna mbili: Kuona kama mfumo

umeundwa na watu kwa ajili ya kuiongoza jamii. Hapa jamii huwa ndio mwanzilishi, mwangalizi na mwelekezaji wa mienendo na masuala mbalimbali muhimu kwa mwanajamii mmojammoja kuelekea kwenye kitovu cha maisha ya ushirika. Pia, ni kuutazama mfumo kwa kuunasibisha na imani kwa miungu. Matakwa ya imani za dini kuhusu himizo la kufanya matambiko, miviga, ibada na sherehe kiushirika ni ushahidi kuwa mfumo huu una mizizi katika masuala ya kiimani. Hivyo, Waafrika walisisitiza maisha ya ushirika kama kanuni ya msingi ya maisha, ujumi na itikadi ya utambulisho wa jamii.

Pili, utu; dhana ya utu ina maana ya kuwa mtu hawezi kuwa mtu bila wengine. Utu ni neno la Kiswahili lenye asili ya Kibantu. Jamii nyingine za Kibantu za Afrika ya Kati, Kusini, Magharibi na Mashariki zinatumia maneno kama Ubuntu, Abantu, Bunhu, Munhu na Umuntu kwa maana hiyohiyo ya utu. Waafrika, kupitia falsafa yao ya utu, wanaamini kuwa mtu huwa mtu kwa kukamilishwa na wengine. Falsafa ya utu inaaminika kuwa ndio msingi wa uhai wa mfumo wa jamii za Waafrika. Kupitia mitazamo ya kiutu, jamii za Waafrika ziliweza kukabiliana na matatizo mbalimbali kama vile ya njaa, mafarakano kati ya ndugu, umaskini na shida mbalimbali kwa kujadiliana, kushirikiana na kusaidiana kindugu.

Tatu, utii na adabu; utamaduni wa Mwafrika umejengwa katika misingi ya kutii na kuonesha adabu kwa mtu yeyote mwenye mamlaka, yaani viongozi na watu wenye umri mkubwa. Enzi za mababu zetu, kutii na kuonesha adabu kwa kiongozi au mwenye mamlaka halikuonekana kama jambo la ukandamizaji au utumwa; lilikuwa jambo la kiujumi. Jamii nzima ilivutiwa na kupendezwa na hali ya kuheshimiwa kwa wenye mamlaka. Kwa upande wa watoto, walipaswa kuwa na adabu kwa wale waliowazidi umri. Mwanajamii yeyote ambaye hakutii ngazi hizo, jamii ilimwona kama mtu asiyefaa na muwi. Ilikuwa nadra kwa hadithi inayosimuliwa kukosa kipengele kinachosawiri hali ya utii na adabu.

Nne, ushababi; hiki ni kipengele cha ujumi wa Kiafrika ambacho huhusisha hali ya ujana/vijana hususani wa kiume ambao huwa na sifa ya ujasiri, uhodari, urijali na ushupavu. Mara nyingi hufungamana na masuala ya sihiri yanayowawezesha kufanya mambo ambayo watu wengine hawawezi kuyafanya. Ushujaa ni sifa iliyopendwa kwa kuwa iliambatana na ukombozi pamoja na ushindi. Hadithi nyingi simulizi za Kiafrika zimesheheni visa vya mashujaa waliokuwa wamefanya vitendo vya kishujaa katika kuzikomboa jamii zao kwenye majanga au kwenye vita. Kwa mfano, shujaa Fumo Liyongo, Lwanda Magere na Kinjekitile katika *Utendi wa Fumo Liyongo*, *Hadithi Fupi ya Lwanda Magere* na *Tamthiliya ya Kinjekitile* mtawalia.

Tano, ukizinda au ubikira; hii ni hali ya kitu, umbo au mtu kubaki katika hali ya uasili wake. Mwali katika utamaduni wa baadhi ya jamii za Kiafrika, hakupaswa kukutana kimwili na mwanamume hadi alipoolewa. Uamuzi wa kufanyika au kutofanyika kwa sherehe za harusi ulitegemea majibu ya jaribio la kupima ubikira. Ubikira ilikuwa ni sifa ya uzuri kwa mwali. Sifa hii ya ubikira katika kazi za sanaa

inawiana na sifa ya ubunifu au upya wa mtunzi katika kazi za fasihi. Ubunifu ni upya na upekee wa kazi ya sanaa. Katika utambaji wa ngano, mtambaji alitumia mbinu mbalimbali ili kuleta upya wa hadithi ikiwamo mbinu ya ufaraguzi. Ubunifu ni sifa ya kiujumi katika kazi za sanaa kama ilivyojadiliwa na mtaalamu Denis Dulton aliyebainisha sifa saba za ujumi katika kazi za sanaa kuwa ni ufundi, kuiga, mwelekeo wa pekee, uzuri usio na tija, ubunifu, mtindo na uhakiki (Dulton, 2001).

Sita, umakusudio; hii ni hali ya umbo au kazi ya sanaa kuthaminishwa kuwa nzuri pale inapotimiza makusudi fulani. Kwa mtazamo wa jamii za Kimagharibi, uzuri ni uwezo wa umbo kuburudisha na kuvutia katika macho ya mtazamaji. Waafrika huuona uzuri wa umbo pale linapoonekana kufaa katika kazi fulani. Msimamo wa makala haya ni kwamba kazi za sanaa zikiwamo hadithi fupi zipo kwa ajili ya kutimiliza makusudio kadhaa ya jamii. Msingi wa Nadharia ya Ujumi wa Kiafrika katika kuifafanua fasihi ni kwamba sanaa ipo kwa lengo la kutimiliza makusudi fulani nje ya sanaa yenyewe. Kulingana na misingi ya Nadharia ya Ujumi Mweusi, ufafanuzi wowote utakaofanywa kuhusu fasihi, hauna budi kuirejelea jamii au mwanajamii ambaye fasihi imekusudiwa kwake. Kazi ya fasihi ina wajibu wa kuelimisha, kuamsha hisia, kutia hamasa, kuonya na kuadilisha. Hivyo, ubora na ujumi wa kazi ya fasihi utapimwa kwa kuangaliwa ufanisi wake katika kuijenga, kuiendeleza, kuistawisha na kuiongoza jamii.

Saba, imani za dini; wataalamu mbalimbali waliojihusisha na uchambuzi wa ujumi katika utamaduni wa Mwafrika pamoja na kazi zao za sanaa, wanakubaliana kuwa sanaa na utamaduni hufungamanishwa kwa kiasi kikubwa na miungu waiabuduyo (Mbiti, 1969; Ozumba, 1995; Mulokozi; 1997). Dini za Kiafrika kwa sehemu kubwa ndizo zimeweka misingi ya maadili katika tamaduni mbalimbali za Kiafrika. Taratibu za kimaadili za Waafrika zinawafanya waonekane ni watu wa kidini sana kwa kuwa kila wanalolifanya hufanya kwa kutumaini na kuhofia walio hai, miungu, mizimu, mungu pamoja na watu waliokufa (Ozumba, 1995). Utambuzi wa lipi ni jambo jema na lipi ni baya, hutambulika kwa kupitia miungu. Hivyo, uzuri au ubaya wa kitu huweza kuamuliwa kutokana na kutambuliwa kwa thamani ya kitu hicho kupitia imani za dini za jamii husika.

## 5.0 Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili

Utanzu wa hadithi fupi simulizi kama ulivyoelezwa hapo juu, una vijitanzu mbalimbali ambavyo hutofautiana kwa majina, dhima, wahusika na maudhui. Ujumi katika vijitanzu hivyo hujipambanua katika vipengele mbalimbali kulingana na dhima kuu pamoja maudhui ya kijitanzu husika. Kwa mfano, kuna vijitanzu ambavyo dhima yake ni kueleza na kukuza tabia za ushujaa, ushupavu na busara katika kupambana na matatizo ya kijamii. Vijitanzu vingine vya hadithi hulenga kutoa mafunzo ya kimaadili katika jamii, kuimarisha itikadi ya jamii kama vile umoja na utu. Katika makala haya tumefafanua na kutoa mifano ya vijitanzu mbalimbali vya hadithi fupi simulizi ili kuonesha ujumi wa Kiafrika katika hadithi hizo. Ujumi wa Kiafrika katika fasihi hufafanuliwa kupitia kategotia za uzuri, ufutuhi, uwi, utanzia na vichekesho. Katika makala haya tumechambua kategoria

ya uzuri pamoja na mpinzani wake uwi, kategoria nyingi hazijahusishwa. Msimamo wa mwandishi ni kuwa uzuri ndio kategoria ya msingi katika ujumi. Kwa muktadha wa makala haya, thamani ya kiujumi wa Kiafrika imetazamwa kupitia hadithi fupi simulizi za Kiswahili.

Uchambuzi juu ya uzuri wa Kiafrika katika hadithi fupi simulizi katika kuonesha thamani za ujumi wa Kiafrika katika makala haya umehusisha vipengele vya umoja, utii na adabu, utu, ushababi, ukizinda, makusudio na imani za dini kama ifuatavyo:

**5.1 Uzuri katika Umoja**

Kabla wakoloni na wageni wengine hawajaathiri utaratibu wa maisha ya Mwafrika, uzuri haukupatikana nje ya maisha ya ushirika. Katika nyanja zote za maisha yaani masuala ya kiuchumi, kisiasa, kielimu, kiulinzi na kiutamaduni; watu waliamini katika umoja. Kwa mfano, katika shughuli za uzalishaji mali kama vile uhunzi, kilimo, uwindaji, ujenzi hata katika sherehe na masuala ya jando na unyago yalifanyika kwa ushirikiano. Mtazamo wao kuhusu ufanyaji kazi ulikuwa chanya, kazi haikutazamwa kama ni shughuli inayoambatana na maumivu bali iliyojaa burudani za kutosha. Kazi zilifanyika kwa umoja na kwa kushirikiana huku zikiambatana na nyimbo pamoja na ala za muziki. Ingawa kiwango cha uchumi kilikuwa duni, hakukuwa na ombaomba mitaani. Vijana au watoto walikuwa ni wa jamii nzima. Matunda ya kazi walizozifanya kila mwanajamii aliyafaidi. Hali hii ya kuishi kiushirika iliwasaidia kukuza hali ya kujali na kujivunia vitu vyao. Kazi kama za uhunzi zilifanywa na jamii fulani maalumu na siri za ufundi katika kazi hiyo zilirithishwa kwa watu wote wa jamii hiyo. Kulikuwa na jamii au koo ambazo zilitengwa kwa shughuli maalumu kama vile shughuli za kutawala, shughuli za matambiko na kuita mvua. Mwanajamii bora alikuwa si yule aliyefanikiwa kuwa na mali nyingi, bali aliyeshirikiana vema na wanajamii wenzake. Furaha na mafanikio ya mwanajamii yalijikita katika kukidhi haja za imani zao na kuishi kijamaa. Ndipo tunaona kuwa fasihi simulizi ya mwanzo haikujulikana mtunzi wake ni nani, bali ilijulikana kuwa ni mali ya jamii nzima. Mtunzi aliona fahari kuunda kazi yake ya kisanaa na ikapokewa na jamii yake na alijali sana nafasi ya heshima aliyopewa na wanajamii kukitamba kipera cha fasihi mbele ya wanajamii wenzake.

Hata tukichunguza lugha za jamii nyingi za Waafrika, huwa katika hali ya wingi hata kama mada au tukio linaloongelewa halipo katika hali ya wingi. Jamii nyingi za Waafrika husalimiana kwa kutumia maneno yaliyopo katika hali ya wingi, hata kama salamu zinaelekezwa kwa mtu mmoja. Kwa mfano, katika jamii ya Wakinga watu wawili wakikutana husalimiana ‘mgonile’ (hamjambo) anayesalimiwa hujibu ‘tugonile’ (hatujambo). Salamu hizo hubeba uwakilishi wa wanafamilia wengine ambao hawapo hapo. Msisitizo wa kuishi maisha ya umoja unadhihirika pia hata katika methali za Waswahili pamoja na misemo: ‘Mkataa wengi ni mchawi’; ‘jifya moja haliinjiki chungu’; ‘mkulima mmoja walaji wengi’; ‘mtu ni wenziwe’, ‘umoja ni nguvu utengano ni udhaifu’; ‘kidole kimoja hakivunji chawa’ na ‘samaki mmoja akioza wote wameoza’.

Suala la umoja au kuishi kwa ushirika ni jambo la kiujumi kwa Waafrika. Hadithi fupi simulizi mbalimbali za jamii za Kiafrika zimekuwa zikisawiri jambo hili kwa namna mbalimbali: Miongoni mwazo ni usawiri wa matendo ya wanyama. Matendo ya wanyama mara nyingi huwa ni ya kibinafsi. Wanyama kama sungura wakati mwingine huonekana kama anawasaidia wenzake lakini hatima yake huishia katika ubinafsi. Sifa za ujanja, ulaghai, uchoyo, hila na unafiki ni za kibinafsi. Matendo haya ya wanyama hutoa funzo kwa jamii kwa kuonesha madhila yanayoambatana na tabia za kibinafsi na uzuri wa maisha ya kushirikiana.

Hurafa ya "Fisi na Rafiki Zake"

> Siku moja fisi alialikwa kwenda kwenye sherehe fulani na jamaa zake. Basi alionelea ni vizuri awaalike marafiki zake katika sherehe hiyo. Wanyama hawa watatu, yaani fisi, sungura na mbwa waliandamana na kuelekea kulikokuwa na sherehe hizo. Walipofika, walikaribishwa kwa mikono miwili na mwenyeji wao. Walipewa vyakula na vinywaji vya kila aina. Baadaye walitumbuizwa kwa nyimbo za kitamaduni. Siku hiyo ilikuwa ya kufana sana kwao. Giza lilipoingia, walionyeshwa mahali pa kulala. Walimolala mlikuwamo na mbuzi na kondoo. Kama tujuavyo, fisi hangeweza kulala kwa ulafi wake. Aliamka usiku wa manane wenzake walipokuwa wamelala usingizi wa pono na kuanza kufikiria juu ya wanyama wale... (King’ei na Kisovi, 2005: 67).

Hadithi hii inaonesha tabia ya uroho ya fisi ya kula kondoo wa mwenyeji wake wakati wenzake mbwa na sungura wamelala usingizi. Pia, hadithi inabainisha tabia ya ujanja ya Sungura ya kumtaja mbwa kuwa ndiye aliyekula kondoo ili kuokoa uhai wake na kifo. Tabia ya uroho na ya ulaghai ni za kibinafsi, zilisambaratisha mshikamano uliokuwapo kati ya mbwa, sungura na fisi. Tabia za ubinafsi kwa mtazamo wa Waafrika ni tabia za kinyama au wanyama. Hii ndiyo sababu kubwa ya kuwatumia wahusika wanyama katika masimulizi haya ili kuweka msisitizo kwamba tabia hizo ni za wanyama na siyo binadamu. Hadithi hii ni kielelezo cha namna jamii za Kiafrika zilivyotegemeana, kuwa karibu na kufungamana sana katika mambo mbalimbali. Fisi ndiye aliyealikwa kwenye sherehe lakini aliamua pia kuwaalika rafiki zake. Alifanya hivyo kwa kuwa sherehe zilichukuliwa kuwa ni jambo la uzuri na la furaha. Uzuri hupatikana katika umoja. Hivyo, kusingekuwa na uzuri wowote endapo fisi angejifungia yeye na wenyeji wake wakaanza kusherehekea kwa kula na kunywa. Kama nadharia ya ujumi mweusi ielezavyo kuwa kanuni na sheria za kuhakiki ujumi wa fasihi zinapaswa kuibuliwa ndani ya jamii yenye kazi husika ya fasihi. Kuna ujumi unaoendana na jamii za kibepari, halikadhalika ujumi unaoendana na jamii za kijamaa. Kwa jamii za kibepari uzuri unapatikana katika ubinafsi ilihali katika jamii za kijamaa ubinafsi ni uwi.

Kupitia hurafa hiyo, tunaiona sifa ya ukarimu kama kiungo cha kuishi maisha ya ushirika kwa Waafrika. Sifa ya ukarimu wakati mwingine imekosolewa hasa inapofungamana na masuala ya mila na desturi za kijamii. Aghalabu jamii nyingi za Kiafrika hutoa kipaumbele cha kumhudumia mgeni kuliko mwenyeji hata kama wote wanamahitaji yanayolingana. Kwa mfano, wakati mwingine mgeni huwatembelea wenyeji wake nyakati za usiku bila taarifa. Kutokana na itikadi za utu za Kiafrika, wenyeji huamua kujinyima au kujipunja katika mahitaji yao ili wamshirikishe na mgeni. Fisi ndiye aliyealikwa kwenye sherehe, naye akaamua kualika rafiki zake wawili ambao mwenyeji wake hakumpa ruhusa ya kufanya hivyo. Yote haya yalifanyika kwa sababu jamii za Kiafrika zinapendezwa na maisha ya ushirikiano.

Maisha ya ushirika huwafanya watu kuwa na moyo wa uzalendo kwa jamii na taifa lao. Huweka mbele maslahi ya jamii na ya taifa lao kuliko matakwa yao binafsi. Utajiri wa mtu mmoja ndani ya jamii maskini huwa sio jambo la kujivunia bali huwa chanzo cha hofu na mashaka. Kufanikiwa kwa jamii, kwa mfano, kimiundombinu, kuwapo kwa chakula cha kutosha, ulinzi imara na utawala mzuri huwa ni furaha na ni uzuri wa wanajamii wote. Uzuri kwa Waafrika hupatikana katika masuala ya kijumuiya na wala sio katika masuala ya mtu mmojammoja.

**5.2 Uzuri katika Utii na Adabu**

Utiifu na kuwa na adabu ni sura ya uzuri katika jamii za Kiafrika. Mwanajamii anaweza kuwa na uzuri wa umbo lakini akakosa kuwa na utii pamoja na adabu, hali hiyo inakuwa ni sawa na nguo nzuri iliyopakazwa uchafu. Sifa hii ya utii na adabu ni ya kidarajia kwa kuwa watoto hutakiwa kuwatii wazazi wao au watu waliowazidi umri na watu wazima huwatii wale wenye mamlaka yaliyo juu yao.
Hadithi ya ngano ya Wakinga ya *Kuchonga Meno*

> ...Wakiwa njiani, wasichana watatu walikuwa wakinywa pombe hiyo na kuongezea maji, lakini mmoja wao hakufanya hivyo. Walipofika, kila mmoja akapeleka pombe yake kwa mjomba. Mjomba wao akaonja pombe ya kila mmoja. Ndipo akawachonga meno vibaya vibaya wote. Mjomba akamnong’oneza msichana aliyepeleka pombe bila kuchakachua kuwa akiache kibuyu chake akifika njiani awambie wenzake kuwa amesahau kibuyu chake, anarudi kukichukua. Alivyorudi peke yake, mjomba wake akatengeneza meno yake vizuri. Msichana huyo akaondoka haraka hadi akaambatana na wenzake. Baada ya kutembea umbali mrefu wakawa wamechoka, walipofika kisimani wakaamua kupumzika. Wakaambiana kuwa, kila mmoja wao acheke ili waone meno yao yalivyotengenezwa na mjomba... (Sanga, 2018: 173-178)

Hadithi hii, inasimulia kisa cha wasichana wanne walioagizwa pombe na wazazi wao ili wakampelekee mjomba wao. Wasichana watatu hawakuonesha adabu wala utii kwa kuwa njiani walikuwa wakinywa pombe ya mjomba wao na kuiongezea

maji, hivyo hawa walikuwa ni wabaya kwa ujumla. Msichana mmoja ndiye aliheshimu agizo la mzazi wake kwa kuipeleka pombe katika uhalisi wake. Baada ya kuwasili wasichana hao, mjomba wao alifurahishwa sana na msichana ambaye alifikisha pombe halisi na akatengeneza meno yake vizuri. Wale watatu waliokosa utii na adabu wakatengenezwa vibaya meno yao. Hivyo, tabia yao mbaya ya kukosa utii ndiyo ilikuja kujitokeza katika mwonekano wa sura zao kupitia meno yaliyotengenezwa vibaya. Meno kwa Wakinga enzi hizo kilikuwa ni kipengele kimojawapo cha idili ya uzuri katika mtu.

Halikadhalika katika Mbazi ya *Ng'ombe na Ndama Wake* (Sanga, 2018) ambayo inasimulia kisa cha baba pamoja na mtoto wake ambao walikuwa wakimsafirisha ng'ombe pamoja na ndama wake katika kijiji cha jirani. Walipofika penye mto, ng'ombe akawa anagoma kabisa kuvuka. Baba akawa anakimbizana naye huku na kule bila mafanikio. Mtoto wake alipoona mateso na jitihada za mzazi wake ambazo hazizai matunda, alimshauri kuwa wambebe ndama wampeleke ng'ambo ya mto kwanza ndipo na mama yake angevuka. Baba, mwanzoni alipuuza ushauri huo wa mtoto wake, na baadaye alipoona ameshindwa kabisa kumvusha ng'ombe, alijaribu kile alichomshauri mtoto wake hapo awali. Alipomvusha ndama ng'ambo ya mto na mama yake bila usumbufu akavuka mwenyewe. Baba yule, baada ya kuona jambo hilo alichanganyikiwa sana, badala ya kumpongeza mtoto wake kwa ushauri wa busara alitokomea porini kwenda kujinyonga. Mbazi hii inathibitisha kuwa utii na adabu ni kipengele cha uzuri kwa Waafrika ukiwa katika ruwaza husika kidarajia na ikiwa kinyume chake inakuwa ni ubaya. Hili linaukilia mawazo ya Zirimu katika Nadharia ya Ujumi Mweusi kuwa tathmini ya ujumi itoke ndani ya jamii na siyo nje ya jamii. Hata hivyo, kulingana na maadili ya Kiafrika, ilikuwa ni vigumu mzazi kumtii mtoto. Mara nyingi iliaminika kuwa busara na hekima hutoka kwa watu wenye umri mkubwa. Watoto huonekana kama hawajui chochote na wanapaswa kuelekezwa kila jambo.

**5.3 Uzuri katika Utu**

Misingi ya utu humtaka mwanajamii kuwatambua, kuwathamini na kuwatendea watu wengine kama ambavyo yeye angependa atendewe na wao. Hivyo, bila wengine mtu hawezi kuwa binadamu aliyekamilika. Utamaduni wa Kiafrika husisitiza wanajamii kuwa na tabia za kiutu kama vile kuonesha upendo, ubinadamu, kujali na kuwa na maelewano na wengine. Hizi ni sifa muhimu katika kujenga jamii inayojali haki na usawa kwa watu wote. Heshima na upendo miongoni mwa wanajamii huchukua nafasi kubwa katika jamii za Waafrika. Kwa Waafrika, utu wa mtu hutambuliwa pale anapoishi maisha yenye misingi ya utamaduni wa kushirikiana.

Hurafa ya "Fisi na Rafiki Zake" ambayo imefafanuliwa hapo juu, imetumia wanyama kueleza na kukemea vikali juu ya vitendo visivyo vya kiutu katika jamii. Fisi alikuwa ni mgeni mwalikwa katika sherehe lakini kutokana na misingi ya Kiafrika ya kuishi maisha ya kushirikiana, naye akawaomba rafiki zake mbwa na sungura waambatane naye. Jamaa yake fisi aliwakarimu wageni wote bila matatizo; walikula, wakanywa na kuburudishwa na nyimbo za kitamaduni na

hatimaye wakaoneshwa mahali pazuri pa kulala. Upo usemi wa Waswahili usemao 'shukrani ya punda ni mateke' na ndivyo alivyofanya fisi usiku ule. Pamoja na kukirimiwa kila kitu katika sherehe ile, kwa kuwa alikuwa mlafi akaamua kula kondoo wa mwenyeji wake kwa siri. Sungura naye kwa sababu ya tabia ya ubinafsi akaamua kumsingizia mbwa kuwa ndiye aliyemla kondoo ilimradi yeye asalimike. Tabia zisizo za kiutu wanasukumiwa wanyama ijapokuwa wanyama huwakilisha tabia za watu na jamii haitarajii watu wafanye hayo. Utu ni uzuri wa mtu na humtofautisha mtu na mnyama.

**5.4 Uzuri katika Ushababi**

Sifa za kishababi zilisisitizwa sana katika jamii hasa vijana ambapo walifunzwa mbinu za kuzifikia sifa hizi. Kwa mfano, katika jamii ya Wamasai, pindi vijana wakiwa jandoni, hufundishwa mbinu mbalimbali za kishababi kama vile kupambana na simba hadi kumuua, na anayefanikiwa kumuua simba na kufanya vitendo kadhaa vya kishujaa alichukuliwa kuwa ni kijana hodari na alipewa cheo cha Morani. Kwa kuwa ushababi ilikuwa sifa ya kiujumi kwa Waafrika, watu wenye sifa hizo walipendwa katika jamii na kupewa heshima ya kipekee.

Mashababi walikuwa ni mashujaa wenye uwezo mkubwa wa kushangaza kiwango cha kutoaminika katika ulimwengu halisi. Upekee wao huanza kutambulika tangu kuzaliwa kwao, kukua na katika kutenda matendo mbalimbali ya kishujaa katika jamii yao. Mashujaa hawa waliweza kuzisaidia jamii zao hasa zilipokumbwa na majanga mbalimbali kama vile njaa, vita, ukame na magonjwa. Aghalabu kila jamii ilikuwa na mashababi wake. Kwa mfano, katika visakale vya jamii ya Wakinga[2], Lwembe ndiye shujaa anayesimuliwa kuwa aliwahi kuwapo.

> Lwembe alikuwa mtoto mmojawapo wa machifu wa Wakinga walioishi eneo la Ukwama ambako kulikuwa ndio makao yao makuu. Lwembe akiwa na vijana wenzake machungani alikuwa akifanya mambo kadhaa yaliyolikuwa yakiwashangaza wenzake. Kwa mfano, mchana wakihisi njaa Lwembe alibadilisha mavumbi yakawa unga wa ulezi na wakapika ugali wakala. Wakati mwingine alikusanya mavi ya mbuzi akaweka kiganjani mwake na yakabadilika kuwa karanga na akawapa wenzake wakazitafuna. Alikuwa pia na zizi kubwa porini lililojaa ng’ombe ambao walitokana na ng’ombe wa kufinyanga udongo ambapo alifinyanga udongo, akapiga kwa fimbo na akawa ng’ombe halisi... (Sanga, 2018: 182-183).

Shujaa huyu alifanya mambo mengi yaliyoishangaza jamii kiasi cha kuleta hofu kwa baba yake ambaye alikuwa chifu. Pamoja na baba yake kupanga mipango ya

---

[2] Jamii ambayo mwandishi aliitafiti kwa kufanya mahojiano kuhusiana na hadithi fupi simulizi. Wakinga asili yao ni wilaya ya Makete, mkoa wa Njombe.

kumuua ili asipokwe nafasi yake, hakuweza kwa sababu Lwembe alikuwa akilindwa na chui pamoja na simba.

Usimuliaji wa hadithi za visakale ulikuwa na manufaa kadhaa katika jamii za Kiafrika. Kwanza, ilikuwa ni kumbukumbu juu ya mashujaa wao, kwa kuwa enzi hizo hakukuwa na maandishi ya kuhifadhi. Hivyo, waliwaenzi na kujivunia jitahada zao kwa kusimulia matendo yao. Pili, visakale viliwafunza vijana kuwa wazalendo kwa jamii zao kwa kuwa mashujaa hao, wengi wao walipambana kwa ajili ya kuziokoa jamii zao. Tatu, iliwachochea vijana kuwa na ndoto na ari ya kutumia vipawa, nguvu na uwezo wao kwa kiwango cha juu ili kuyafikia malengo mbalimbali. Kwa kuwa mashujaa wengi miisho yao haikuwa mizuri aghalabu wengi walitegeshewa mitego ya wanawake warembo na jamii pinzani ili wawahadae, hivyo, hadithi hizi ziliwasaidia vijana kujifunza kupitia makosa yao. Nne, ilikuza moyo wa kujiamini kwa wanajamii wa jamii ya shujaa huyo dhidi ya jamii za karibu yao, hasa shujaa huyo anapowashindia vita.

**5.5 Uzuri katika Ukizinda**

Ukizinda ni hali ya kitu kuwa na upya. Dhana ya ukizinda ina mitajo tofautitofauti kulingana na madaraja ya tathmini ya uzuri wa kiujumi. Kwa mfano, kwa mtu hasa mwanamke ukizinda humaanisha ubikira. Ukizinda katika asili humaanisha asili ya kitu na siyo upya, mathalani, hali ya mtu kuvutiwa na mitumba kuliko vitu vipya. Katika kazi za sanaa ukizinda humaanisha upya utokanao na mbinu za kiubunifu.

Uzuri katika ukizinda unaonekana na umeelezwa pia katika ngano ya jamii ya Wakinga ya “Kuchonga Meno” tuliyoielezea hapo juu. Wasichana watatu katika wanne walioagizwa kupeleka pombe kwenye vibuyu kwa mjomba wao, walishindwa kuipeleka katika uasili wake. Waliipunguza kwa kunywa na kuiongezea maji. Jambo hilo lilimkera sana mjomba wao mpaka akafanya uamuzi wa kuwatengeneza meno yao vibaya. Pombe ya wasichana watatu iliyopelekwa kwa mjomba wao ilikuwa bado imejaa katika vibuyu lakini ilikuwa imepunguzwa na kujazwa maji. Kitendo cha kupunguza pombe na kuongeza maji kiliondoa hali ya uasili wa pombe hiyo; ijapokuwa ilibaki kuwa pombe lakini haikuwa nzuri.

Uzuri wa ukizinda pia unadhihirika katika upya unaojitokeza katika kazi za fasihi. Hekaya ni miongoni mwa hadithi fupi ambazo zilikuwa zimebeba upya wa kimawazo katika kutatua masuala mbalimbali ya kijamii. Hekaya ni hadithi ambazo husimulia juu ya wahusika wajanja ambao aghalabu huwahadaa wahusika wengine na kunufaika. Wahusika hao huweza kuwa ni wanyama, watu au mchanganyiko. Hekaya ni hadithi zenye visa vya kusisimua na kustaajabisha. Hadithi ya “Mzee Kobe na Sungura” inaelezea ujanja na ubunifu wa kobe uliokomesha chokochoko za sungura juu ya jamii ya wanyama wenzake porini.

> ...Sungura hoyee! Aliyarudia maneno yake na kuendelea. Nani asiyemjua sungura katika mbuga hii? Hivi majuzi tu nilimshinda chui katika mbio za nyika! Kwa sasa, namtaka Duma athubutu kushindana nami. Nimesikia madai ya

> kipuuzi kwamba huyu ndiye mkimbiaji hodari zaidi ya wanyama wote. Hebu mtafuteni kati yenu!"Alizidi kudharau. Wanyama wote walitazamana. Duma hakuweko mkutanoni. Hata mfalme wao simba alishtushwa na jambo hili. "Msipoteze muda kulitafuta! Duma ni jinyama jioga lisilofua dafu mbele yangu!"Sungura alisema huku akirukaruka kwa furaha. Ni nani bingwa sungura aliuliza kwa sauti ya juu."Sungura ndiye bingwa! Wengi wa mashabiki wake walishangilia... (M'ngaruthi, 2008:40-43).

Sungura ni mnyama anayesifika kuwa mjanja kuliko wanyama wote wa porini kwa jamii mbalimbali za Afrika Mashariki. Hadithi hii inaeleza kuwa sungura alionekana kuwa ni mnyama bingwa katika mbio za nyika. Ubingwa huo ulimfanya sungura kuwa na majigambo huku akiwatusi na kuwafedhuli wanyama wenzake hususani wanyama wakubwa kwa umbo kama chui, duma, mbweha na mbwa mwitu. Hata hivyo, ubingwa wenyewe wa mbio za nyika ilionekana anaupata kwa ujanjaujanja tu. Wanyama wengi walikuwa wakisikitika na kufadhaika na matusi ya sungura kwao, wasijue kitu cha kufanya. Mzee kobe aliomba apangwe na sungura kushindana mbio za nyika. Jambo hilo lilionekana kituko kwa wanyama wengi akiwamo sungura mwenyewe. Sungura alijua daima mzee kobe ni mnyama mzembe. Jambo lililowashangaza wanyama wote pale mzee kobe alipoonekana amekuwa wa kwanza katika mashindano hayo na kumwacha sungura nyuma sana. Ujanja aliotumia mzee kobe ambao wanyama wengine hawakujua wa kupanga kobe sita katika vichaka vya njia inayotumiwa kwa mashindano ndio ulimwangusha sungura. Ubunifu huo wa mzee kobe ndio ulimfanya apendwe na wanyama wengine kwa kuwa yeye ndiye aliyewakomboa kutoka kwenye manyanyaso ya sungura. Sungura alijiona kuwa kiumbe dhalili sana baada ya kushindwa kung'amua mbinu aliyotumia mzee kobe kumshinda. Kwa sababu mzee kobe mara zote katika mbio za nyika alikuwa akishika nafasi ya mwisho na sasa amemshinda bingwa wa miaka yote.

Sifa ya ubunifu ni ya kiujumi na ilikuwa ikitambuliwa katika jamii za Kiafrika. Watambaji wa hadithi fupi simulizi aghalabu walijitahidi kuongezea vitu vya kiubunifu wakati wa kusimulia hadithi ili kuleta upya katika hadithi hizo, kwa sababu mara nyingi walikuwa wakizikariri hadithi zilezile. Hili linayakinishwa na Nadharia ya Ujumi Mweusi inayopinga wageni ambao hawana uzoefu na taarifa za kutosha kuhusu Afrika na Waafrika kuhusu kazi zao za fasihi, kuwa mstari wa mbele katika kuhakiki thamani za kiujumi za kazi hizo. Kwa mfano, mwanaisimu Mwingereza, Richard Burton, aliyefanya kazi kama mfasiri katika jeshi ambaye alifanya utafiti Afrika Magharibi kwa miaka miwili tu na akaandika kitabu cha *Wit and Wisdom from West Afrika* (1865). Burton alikusanya nahau na methali za Afrika Magharibi na anasema kuwa Afrika hakuna ushairi, hakuna mizani, hakuna vina na hakuna chochote kinachokonga na kugusa moyo.

**5.6 Uzuri katika Umakusudio**

Msingi wa kipengele hiki ni kwamba, kitu huwa kizuri kutokana na sifa ya kukidhi haja ya kazi iliyotarajiwa kifanye. Huu ni uzuri unaopatikana wakati kitu kimetimiza makusudio ya kuundwa kwake. Kwa mfano, uzuri wa jembe huonekana wakati wa kulima. Uzuri huu siyo wa umbo wala mvuto wa kihisia bali ni uzuri wa kutimiza malengo yanayotarajiwa. Vinyago vilivyochongwa na jamii za Kiafrika kipindi kabla ya kuja kwa wageni kutoka mabara mengine vilibeba tafsiri ya Waafrika juu ya ulimwengu usioonekana. Vinyago vingi vilisawiri falsafa ya Waafrika juu ya maisha na imani zao kwa miungu. Vinyago vingi vilikuwa na sura mbaya, hata baadhi ya maski ambazo zilivaliwa katika sherehe mbalimbali zilikuwa na sura ya kutisha. Pamoja na hali ya vinyago hivyo kuwa na sura mbaya, bado vilionekana ni vizuri kwa kuwa vilibeba maudhui kadhaa muhimu kwa jamii.

Hadithi ya kisakale cha “Lwembe wa Wakinga” inasimulia juu ya uwezo aliokuwa nao Lwembe wa kufinyanga ng’ombe wa udongo akampiga na fimbo akawa ng’ombe halisi. Pia, alikuwa akichota vumbi ardhini na akaweka kwenye viganja vyake linageuka kuwa unga na watu wakasonga ugali wakala. Vitendo hivyo vilimfanya apendwe sana na jamii iliyomzunguka, kwa kuwa uwezo wake ulikuwa kama wa miungu. Kitendo cha jamii ile kuanza kumwamini na kumsifia kiliibua wasiwasi kwa baba yake Lwembe, kiasi cha kuhisi kupinduliwa madaraka yake. Hivyo, uzuri wa Lwembe ulikuwa ni wa kimakusudio, ulitokana na kazi alizokuwa akizifanya.

Hadithi ya “Sungura na Mzee Kobe” ambayo nimeielezea hapo juu, inasimulia namna sungura alivyokuwa akijigamba na kushangiliwa na wanyama wenzake. Sungura alijipatia umaarufu katika wanyama wa porini kwa kuwa alikuwa bingwa wa mbio za nyika. Mzee kobe kila mashindano yalipotokea, alikuwa akishika mkia. Kwa sababu hiyo, alikuwa akidharauliwa na kila mnyama na alionekana mzembe siku zote. Hata siku mzee kobe alipoomba kibali cha kushindana na bingwa sungura kwa mfalme, kila mnyama alicheka. Sungura alikuwa mnyama mdogo sana kwa umbo ukilinganisha na tembo, chui, nyati, mbweha na wengine. Hivyo, haikuwa rahisi kujulikana na kusifiwa kupita wanyama wengine. Sifa za ujanja na mbio ndizo zilizoupaisha uzuri wa sungura. Hata hivyo, majigambo na uzuri wa sungura uliporomoka siku waliposhindana mbio za nyika na mzee kobe na sungura akashindwa. Imeeezwa hapo juu kuwa hadithi za hurafa hutumia wahusika wanyama kuelezea tabia na matendo ya watu. Wapo watu wengi sana katika jamii zetu wenye mfano kama wa sungura, ambao uzuri wao ni wa kimakusudio na nje ya hapo hakuna uzuri. Kwa mfano, watu wenye nyadhifa na wenye umaarufu fulani katika jamii. Watu hawa wanapokuwa wameondolewa kwenye nafasi zao mara nyingi hurudi kuwa watu wa kawaida na uzuri wao huporomoka. Uzuri wa kimasudio ni uzuri unaokwenda sambamba na malengo au mahitaji, na hitaji likikamilika na umuhimu wa mtendaji au kitendaji huishia hapo. Uzuri wa kitu hicho huishia hapo na uwi huchukua nafasi yake. Kutokana na misingi ya Nadharia ya Ujumi Mweusi kuwa kila jamii ina namna yake ya kuuhakiki ujumi katika mazingira yake. Kwa kuwa kitu kizuri kwa jamii fulani

siyo lazima kiwe kizuri kwa nyingine. Kwa mfano, jamii za watu wa mataifa ya Mashariki zinatambua thamani za wanyama mbalimbali kama nyoka na hivyo huvutiwa nao. Hii ni kinyume na baadhi za jamii za Waafrika ambao humwona nyoka ni muwi na ni shetani.

Kwa jumla, sanaa za Kiafrika kwa sehemu kubwa ni za uzuri wa kimakusudio. Kwa mfano, hadithi fupi simulizi hazikusimuliwa kila wakati, kulikuwa na wakati maalumu wa kusimuliwa hasa wakati wa jioni baada ya kurejea kutoka kwenye shughuli kama za kilimo, uvuvi, uhunzi na uwindaji. Hata nyimbo na ngoma ziliimbwa na kuchezwa kwenye matukio maalumu. Haikuruhusiwa kutamba hadithi wakati wa mchana, ilikuwa ni jioni baada ya kazi za mchana. Lengo la kutamba hadithi hizo nyakati za jioni baada ya kazi lilikuwa ni kuwaburudisha baada ya kazi ngumu na nzito za mchana. Hali hiyo iliwasaidia kusahau taabu zote walizokabiliana nazo mchana na iliwawezesha kuamka siku iliyofuata wakiwa ari mpya ya kufanya kazi. Katika maktadha huo utambaji wa hadithi unakuwa ni wa kimakusudio.

**5.7 Uzuri katika Imani za Dini**

Ujumi wa Waafrika au Waswahili katika imani za dini ulijumuisha suala la kuabudu miungu, miviga, matambiko na shughuli zilizowapatia watu riziki. Pia, Waafrika huamini ushirikina na kuwa kuna uchawi, na ili mtu aweze kupona anapaswa awaendee waganga wamkinge. Waganga wa kienyeji nao huwasiliana na mizimu, na mahoka katika kuwatatulia watu matatizo. Hili linajidhihirisha pia kupitia hatua zilizochukuliwa katika malezi ya mtoto ambapo ilihitaji afanyiwe miviga na matambiko ili asije akaathiriwa na watu wabaya.

Wazee na watu maarufu waliokufa zamani, hawa waliaminika kuwa hubadilika kuwa mizimu ambao huwa kama kiungo kati ya binadamu na miungu (Mbiti, 1975). Wapo pia watu maalumu ambao husadikika kuwa huwasiliana na hiyo mizimu, hawa ni kama vile waganga wa kienyeji na waaguzi. Miungu hao waliaminika kuwa ndio waliowapatia watu uzao, mema, mvua, kisasi na ukame. Imani hizi za dini zilichangia kwa kiasi kikubwa kujenga na kudumisha maadili katika jamii. Iliaminika kuwa mtu akikiuka miiko fulani ya jamii, miungu ingeweza kumwadhibu. Lwembe aliaminika kama mtu shababi kwa jamii ya Wakinga enzi hizo, kama ilivyoelezwa katika Kisakale cha "Lwembe wa Wakinga". Hadi hivi leo baadhi ya koo za Wakinga huenda eneo la Mwakaleli, mkoani Mbeya, kufanya matambiko ya kuomba mvua kwa Lwembe pale zinapochelewa kunyesha.

Kupitia imani za dini, wanajamii walilazimika kuishi maisha ya kushirikiana, kuwa watiifu na kuheshimiana na kujali utu. Haya yalifanyika kama utekelezaji wa yale yanayoagizwa na miungu yao. Mwanajamii yeyote aliyeonekana kumtendea mwenzake vitendo vya kinyama iliaminika kuwa angeadhibiwa na miungu. Hili linathibitika hata katika hadithi ya "Lwembe wa Wakinga" ambaye alifika katika nyumba ya mkazi mmoja huko Tukuyu, akamwomba maji ya kunywa na alipokataliwa, miungu ilimwadhibu. Ardhi yote ya eneo la mkazi huyo

ilididimia na kukajitokeza ziwa mahali hapo. Pia, shujaa Lwembe aliweza kutoroka kwa nguvu za kiungu katika gereza alilofungiwa na baba yake ili auawe. Alipokuwa akitoroka kutoka eneo la Ukwama-Makete kuelekea Tukuyu, kwa kuwa mahasidi wake walikuwa wakimfuata nyuma, miungu ilimkinga kupitia wanyama wakali. Pia, Lwembe kwa uwezo wa nguvu za miungu aliweza kufinyanga ng'ombe wa matope na akapiga na fimbo yake akawa ng'ombe halisi. Lwembe aliweza kukusanya mavi ya mbuzi na akayaweka katika viganja vya mikono yake na yakageuka kuwa karanga. Pia, kwa uwezo huohuo wa miungu alibadilisha vumbi kuwa unga.

Kazi nyingi za kisanaa za Kiafrika zimeundwa kiishara na nyingi zilikusudiwa kukidhi haja za kimawasiliano na miungu yao (Ojo, 1989 na Mbiti, 1975). Hadithi fupi nyingi za jamii za Waafrika zilizosimuliwa zilisheheni sifa za uwezo na wema wa miungu yao. Hadithi hizo zilionesha nanma miungu hiyo ilivyowapigania na kuwaokoa wanajamii mbalimbali katika nyakati walizokuwa wanakabiliwa na hatari.

Imani za dini kwa jamii nyingi za Waafrika ni suala la kiujumi. Wakati mwingine hata uzuri wa mtu hupimwa kwa kigezo cha namna anavyomudu kutekeleza imani ya dini yake. Uzuri wa vitu, vyakula, wanyama hata kazi za sanaa ulithaminishwa kulingana na tafsiri pamoja na matumizi yake katika kutekeleza masuala ya kidini. Kwa mfano, katika jamii ya Wakinga kondoo mweusi ni mnyama mwenye thamani kubwa kwa sababu hutumiwa katika matambiko. Pombe nayo hupewa thamani kubwa kwa kuwa hutumiwa katika matambiko na sherehe zinazohusiana na matambiko hayo.

**6.0 Hitimisho**

Suala ambalo siyo la kubahatisha ni kwamba umbali uliopo baina ya ujumi wa Kiafrika na fasihi simulizi ya Kiswahili unazidi kuongezeka siku hadi siku. Kipindi hiki cha utandawazi tunashuhudia kupotea kwa masuala muhimu yanayofungamana na ujumi wa Kiafrika. Kupitia tanzu mbalimbali za fasihi, masuala yaliyokuwa ya uzuri na muhimu yalisisitizwa kwa kurudiwarudiwa katika kazi za fasihi zikiwamo nyimbo na hadithi fupi simulizi. Fasihi ilibeba maudhui yanayosisitiza ushababi, umoja, utu na kuheshimiana. Mambo hayo muhimu kwa ustawi wa jamii zetu hatuyaoni katika kazi za fasihi za sasa.

Makala haya hayakusudii kukumbatia ukale na kuubeza usasa ambao unaogelea na kustawishwa na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia. Kila jamii ya watu katika ulimwengu ina namna yake ya kujitambulisha kwa wengine, kuyatafsiri maisha na mazingira yanayowazunguka na kueleza hisia zao katika matukio, hali na matendo katika maisha yao ya kila siku. Yapo mambo muhimu ndani ya fasihi simulizi ya Waswahili ambayo yalipaswa kuumbwa upya ili yaendane na dunia ya sasa. Hadithi fupi simulizi kwa kiwango fulani zinasimuliwa katika vyombo mbalimbali kama vile televisheni na redio. Pamoja na kwamba zinasimuliwa kwa kiasi kidogo, bado hazijabeba ujumi wa Kiafrika ndani yake. Fasihi simulizi ya Kiswahili ndio msingi wa fasihi andishi ya Kiswahili. Ujumi wa Kiafrika ukipotea

au kukengeushwa katika fasihi simulizi bila shaka hata fasihi andishi itapoteza mwelekeo.

**Marejeleo**


Bello, S. (2010). "Communication and Cultural Promotion for Sustainable Development: The Challenges of Globalization," katika Semiu Musa Bello and Adesemoye (2012) Western Films and Teenagers in Nigerian Societies: The Question of Cultural Promotion, Continental journal of Arts and Humanities, Vol. 4(2).

Berrian, A.H. na Long, R.A. (1967). *Negritude*: *Essay and Studies,* Hampton Institute Press, Hampton Virginia.

Burton, R.F. (1865). *Wit and Wisdom from West Africa, or a Book of Proverbial Philosophy, Idioms,Enigmas, and Laconism*. Tinsley Brothers. London

Dutton, D. (2001). *Aesthetic Universals.* Iliyopakuliwa tarehe 23/01/2015 katika www.denisdutton.com.

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology*: *Method and Techniques* (toleo la 2), New Age International Publishers, New Delhi.

Madumula, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Mture Educational Published Limited, Dar es Salaam.

Mbiti, J. (1975). *Introduction to African Religion (toleo la 2),* Nairobi: East Africa Educatinal Publishers.

Mbiti, J. (1969). *African Religion and Philosophy*, Heinemann, London.

M'Ngaruthi, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mulokozi, M.M. (1997), *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*, ECOL, Morogoro.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.

Neugebauer, C. (1991). "The Racism of Hegel and Kant", katika Oruka, H. O. (Mh.), *Sage Philosophy*. Nairobi. English Press.

Ojo, O.J. (1989). "Art in Traditional African Culture". katika Richard O. (Mh.), *African History and Culture.* Lagos: Longman, 200-236.

Ozumba, G.O. (1995), "African Ethics," katika Uduigwomen, A. F (Mh), *Footmarks on African Philosophy*, Oborah and Ogbinaka Publishers, Lagos. Journal of Black Psychology, 29, 3-16.

Samwel, M. (2012). *Hadithi Fupi: Nadharia, Mbinu na Mifano*. Kasenyenda Tanzania, Iringa.

Sanga, N.A. (2018). "Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika hadithi Fupi Andishi za Kiswahili Kipindi cha Utandawazi: Mifano kutoka Magazeti ya Habarileo, Nipashe na Mwananchi", Tasinifu ya Uzamivu. (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Sanga, A.N. (2012). "Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano kutoka kwa Muhammed Said Abdulla na Eristablus Elvis Musiba," Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi, Mfululizo wa Lugha na Fasihi*. KAUTTU. Dar es Salaam.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wamitila, K.W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. English Press. Nairobi.

Zirimu, P. na Gurr, A. (1973). *Black Aesthetics: Papers from a Colloquium Held at the University of Nairobi, June 1971*, East African Literature Bureau, Nairobi.